



THE  
LUTHERAN  
WORLD  
FEDERATION

A Communion  
of Churches

[lutheranworld.org](http://lutheranworld.org)

## UJUMBE WA IJUMAA KUU: KRISTO MSALABANI AMEYACHUKUA PIA MAUMIVU YETU

### Makamu wa Raisi Urmas Viilma, Askofu Mkuu, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Estonia

*Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako.  
Yesu akamwambia, Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami  
peponi (Luka 23:42-43)*

Wakati fulani, katika bustani ya Edeni nyoka alidanganya kuwa hakukuwa na kifo. Lakini bado kikawepo. Leo adui wa kiroho anaendelea kudanganya na kusema kuwa hakuna maisha, na kwamba kifo ndio mwisho wa yote. Lakini bado kipo! Yesu aliuumbua uongo huu akithibitisha kuwa kuna maisha na kwamba umilele si picha ya kufikirika tu bali ni kitu cha kweli chenye mashiko.

Hata kwa mhalifu pale msalabani, Yesu alithibitisha kuwa hakabiliani na kitu kifo kisicho julikana na cha kutisha tu. "Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi," ni maneno ya matumaini, ambayo Yesu alisema kwa mtu aliyekuwa amehukumiwa na kuachwa na ulimwengu.

Ulimwenguni kote kifo ndicho kinachoogopwa sana lakini wakati mwengine kinatarajiwa. Mtu anayeamini anatamani kuwa na Mungu kwa sababu ni afadhali zaidi huko. Akitafakari juu ya kuachana na enzi hii, Mkristo pia anatafakari juu ya ufufuo wa Kristo. Msalaba uliotupu pale kaburini unatukumbusha kuwa maisha yameshinda kifo. Yesu hakubaki msalabani. Yesu hakubaki kaburini pia.

Ni vigumu kwa wale wasio na imani kuelewa juu ya habari njema ya msalaba na kaburi viliviyotupu, kwani hawawezi kuona matumaini ya maisha ya milele. Leo, ebu tuwe na upendo wa kushirikishana tumaini hili kwa wale ambao hawana tumaini hilo. Kifo si jibu. Jibu halisi ni maisha.

Mtume Petro alisema katika hubiri lake la Pentekoste kuwa Mungu alimuinua Yesu, baada ya kuufungua uchungu wa mauti (Mdo 2:24). Hatujui uchungu wa mauti ni nini, kwa sababu hatujui jinsi kifo kilivyo. Sana sana tunajaribu kuhisi kuwa ni kitu chenye maumivu mabaya zaidi - ambayo mwili unayasikia au ambayo nafsi inayasikia. Yesu amekuja ili kuingia katika vita dhidi ya mashaka ya dunia hii yaliyo mabaya na magumu. Kifo msalabani si mchezo wa kuigiza bali ni tendo la maumivu ya kweli. Vivyo hivyo, furaha ya

kweli inahisiwa kwa sababu ya Bwana Mfufuka anayetaka kutupa zawadi ya maisha bila maumivu. Yeye ameyachukua maumivu yetu [yote] pale msalabani.

Je tupo tayari kukubali uzima huu wa milele usio na maumivu? Je yule mhalifu alikuwa tayari kupelekwa na Yesu Paradiso? Ndio, kwa vyovyote vile! Kwa njia hiyo hiyo, hata sisi katika Ijumaa Kuu tunaisubiria asubuhi ya Pasaka inayokuja na ujumbe huu wa Mfufuka: *nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu* (Ufunuo 1:18)

Mungu atusaidie, ili furaha ya Bwana Mfufuka iweze kujaa katika moyo wa kila mtu na pasiwepo mtu wa kuachwa bila furaha. Kama ilivyokuwa kwa mhalifu pale msalabani, sisi wote tumetenda dhambi. Lakini bado tunatamani rehema ya Mungu ambaye ameona masumbuko yetu makali na amesikia maombi yetu. Kwa njia ya Ufufuo wa Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, Mungu ametupa imani na tumaini, kwamba siku ya kufa kwetu, Mungu anatusubiria katika ufalme wake, ambamo sisi wote na wale wote walio na imani watacaa pamoja na Mungu Paradiso.

*Askofu Mkuu Urmas Viilma ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Estonia. Ni Makamu wa Raisi wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), eneo la Ulaya ya Mashariki na Kati.*